JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS - TAMISEMI

Namba za simu

Mkuu wa shule 0763-814313/0787-738415

Makamu Mkuu wa Shule 0787-285747/0764-317021

Matron 0752-984655/0783-072609

Shule ya Sekondari MSALATO

S.L.P 933

Tarehe 17/05/2018

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi.....

.....

S.L.P.....

.....

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MSALATO HALMASHAURI YA JIJI DODOMA MKOA WA DODOMA MWAKA 2018

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano katika shule hii mwaka 2018 tahasusi ya ..... Shule ya Sekondari Msalato ipo umbali wa kilometa 10 kaskazini mwa mji wa Dodoma. Usafiri wa basi kutoka mjini Dodoma unapatikana katika kituo cha mabasi Jamatini nauli ni shilingi 500/= tu.

Muhula wa masomo unaanza terehe 2/07/2018. Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 1/07/2018. Mwisho wa kuripoti ni tarehe 2/07/2018.

2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

2.1 Sare ya shule

a) Kwa wasio waislam: Shati mbili nyeupe za mikono mifupi na mfuko upande wa kushoto. Sketi 2 mavazi ya darasani yenye rangi ya bluu bahari na marinda yanayoangalia upande mmoja yaliyolingana kati ya 13-15.

b) Kwa waislam: Rangi ya hijab (juba) ni nyeupe isiyo na urembo. Suruali mbili za bluu bahari na nusu kanzu nyeupe.
c) Sare ya michezo kwa shule hii ni track suit nyeusi/ dark blue yenye mistari nyeupe pembeni na raba nyeupe.
d) Jezi nyeupe yenye strips nyeusi isiyo na kola.
e) Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.
f) Soksi jozi mbili nyeupe za shule
g) Sweta 2zenye rangi nyeusi na shingo ya **V** mbele.
h) Nguo za kushindia

- Kwa wasio waislam: ni sketi 2 rangi ya damu ya mzee (marloon) iwe kitambaa kizito, mshono wa ndoo au solo inayofunika kifundo cha mguu ambayo siyo pana sana. T-shirt 2 ambalo ni vazi la nje ya darasa yenye shingo ya mviringo, iwe na rangi ya kijivu au nyeupe iliyo na nembo ya shule (atainunua shuleni).
- Kwa waislam: suruali 2 za damu ya mzee (marloon) iwe kitambaa kizito na juba T-shirt 2 ambalo ni vazi la nje ya darasa yenye shingo ya mviringo, iwe na rangi ya kijivu au nyeupe iliyo na nembo ya shule (atainunua shuleni).

i) Tai 2 ndefu ya pundamilia yenye rangi ya kitambaa cha shule (atainunua shuleni).

2.2 Ada na michango ya shule

a) Ada ya shule kwa mwaka ni shilingi 70,000.00. unaweza kulipa shilingi 35,000.00 kwa muhula au kulipa ada yote kwa mara moja. Fedha hizo za ada zilipwe kwenye akaunti ya shuleMSALATO SEC. RUZUKU ACCOUNT Na. 50501100161 katika benki ya NMB. (Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip).

b) Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni:-

Michango mingine ilipwe kwenye akaunti MSALATO GENERAL ACCOUNT Na. 50502800001 katika banki ya NMB (Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip).

i. Shilingi 15,000/= kwa ajili ya ukarabati wa samani.
ii. Shilingi 6,000/= kwa ajili ya kitambulisho na picha.
iii. Shilingi 20,000/=kwa ajili ya taaluma.
iv. Shilingi 30,000/= kwa ajili ya kuwalipa wapishi, walinzi na vibarua wengine.
v. Shilingi 2,000/= nembo ya shule.
vi. Shilingi 10,000/= kwa ajili ya huduma ya kwanza tshs. 5,000/= na Bima ya afya Tshs. 5,000/= (Wanafunzi washauriwe kujiunga na Mfuko wa Bima ya Afya CHF kikaya)
vii. Shilingi 20,000/= Mitihani ya kujipima mock

viii. Shilingi 10,000/= kukodisha godoro kwa mwaka (isiwe lazima)
ix. Fedha ya tahadhari 5,000/= (haitarejeshwa)

Angalizo: jumla ya ada na michango ni 188,000/=

c) Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni:-

i. Ream ya karatasi 1 (kwa mwaka)
ii. Mwanafunzi anashauriwa kuja na hela kwa ajili ya ununuzi wa vitabu vya masomo ya tahasusi husika baada ya kupata ushauri wa mwalimu wa somo husika
iii. Dissecting kit kwa wanafunzi wa Biolojia
iv. Scientific calculator
v. Godoro atapata shulenikama ilivyooneshwa kipengele **2.2 b)** viii
vi. Mashuka jozi 2 (pinki), blanketi 1, foronya 1, chandarua 1 yenye ukubwa wa futi 3 au 4 ya square ambayo ni nyeupe, taulo na jozi moja ya khanga/kitenge. (nguo nyingine zisizo sare ya shule haziruhusiwi)
vii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli,na kikombe visiwe vya plastiki, kijiko na chombo safi cha kuhifadhia maji ya kunywa.
viii. Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko
ix. Kwanja 1, jembe 1, reki 1, mifagio ya ndani na nje
x. Aje na sabuni za kuogea na kufulia, mswaki na dawa ya meno, mafuta ya kupaka, losheni, pedi za kike,skin taiti, sidiria iwe nyeupe au nyeusi tu.
xi. Sanduku la chuma (tranka) , tochi na betri au tochi ya sola na pia aje na sare ya shule alikotoka kabla hajapata sare rasmi ya shule hii kwa wale ambao watakuwa hawajashona.

3. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

(i) Wizi
(ii) Kutohudhuria masomo kwa Zaidi ya siku 90 bila taarifa/ utoro.
(iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo
(iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/ walezi na jamii kwa jumla.
(v) Kupigana mwafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote yule.
(vi) Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wotw wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule.
(vii) Kufuga ndevu
(viii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya
(ix) Uvutaji wa sigara.
(x) Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa.
(xi) Kupata ujauzito au kutoa mimba

(xii) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sharia za nchi
(xiii) Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana
(xiv) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
(xv) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule
(xvi) Kudharau Bendera ya Taifa
(xvii) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
(xviii) Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

4. Viambatisho na Fomu Muhimu

a) Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya serikali. (imeambatishwa ukurasa wa 6)
b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/ mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai. (mkataba huu utapatikana shuleni)
c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni, kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule. (imeambatishwa ukurasa wa 5)
d) Picha nne (4) za Wazazi na Ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu

MUHIMU

5. Baada ya kupakua (download) fomu hii, tafadhali jaza jina la mwanafunzi na anwani yako pamoja na tahasusi aliyochaguliwa kusomea hapa Sekondari ya Msalato. Hakikisha unajaza tahasusi (combination) aliyopangiwa na serikali. Taarifa hizi zijazwe kwenye ukurasa wa kwanza.
6. Mwanafunzi atakaporipoti shuleni aje na fomu hii pamoja na result slip ya kidato cha nne.
7. Tafadhali soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA MSALATO SEKONDARI

LINE CHANAFI
MKUU WA SHULE

HEADMISTRESS
MSALATO SECONDARY SCHOOL
P.O. Box 933
DODOMA

OR – TAMISEMI
MANISPAA YA DODOMA

SHULE YA SEKONDARI MSALATO
FOMU YA KUKUBALI SHULE

A. SEHEMU YA MWANAFUNZI

1. Mimi (Majina kamili) ……..
   Nimekubali kuingia kidato cha …… katika Shule ya Sekondari Msalato Dodoma kuanzia tarehe …… hadi nitakapomaliza kidato cha ……
2. Naahidi kwamba nitatii sheria za Shule na kushiriki katika shughuli zote za shule kikamilifu kulingana na ratiba.
3. Tarehe ya kuzaliwa……. Kijiji……...
   Tarafa……... Wilaya ……...
   Shule unakotoka ……...Namba yako ya mtihani……
4. Kituo cha gari (Bus) au Gari la Moshi kilichopo karibu na nyumbani kwako…….
5. Nikimaliza kusoma shule ningependa kufanya kazi ifuatayo ……

   Sahihi ya mwanafunzi ……. Tarehe ……...

B. SEHEMU YA MZAZI AU MLEZI

1. Mimi (majina kamili) …… ninakubali mtoto wangu asome katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Msalato kuanzia kidato cha ……hadi atakapomaliza kidato cha ……. Nakiri kukubaliana na sheria,kanuni,kulipa ada,michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
2. Jina kamili la Mama …… Jina kamili la Baba…….
3. Kazi ya Mama ……Kazi ya Baba ……
4. Anwani ya Mzazi/Mlezi ……
   ……
5. Wafuatao ni Ndugu zake ninaowatambua wanaishi hapa Dodoma na wanaweza kumsaidia wakati wa dharura

   Jina kamili Mahusiano Anakoishi Simu yake

   (i)……..... ...……..……. .....…….....
   (ii)……..... ……..……..... .. ……..... .....…….....
   (iii)……..... …… ...……..... ..... ……..
   (iv)..... ....
6. Madhehebu ya Dini ya Mtoto ni Lutheran/Katoliki/Anglican/PAG/TAG/ Moravian /SDA/Mwislam

7. Ripoti zote za maendeleo ya mwanafunzi ziwe zinatumwa kwa
   ……..
   ……..
   Saini ya Mzazi/Mlezi ..... Tarehe ……

MSALATO SECONDARY SCHOOL
FORM FOR STUDENTS MEDICAL EXAMINATION

To be completed by a Medical Officer

…… (Insert name of **the** Government Medical Institution)

Name of Student …… Form …… Year…….

Age……Sex……

Blood count…….

Stool ……

Urine ……

T. B. Test…….

Eyes……

Ears…….

Chest……....

Spleen ……

Abdomen……

Teeth ……....

Additional information: - (***e.g. pregnancy, physical defects, infections, psychological disorder, chronic or family diseases).***

…….....

……
……

I certify that above pupil is fit to continue with studies in Secondary School for two years.

Name of Medical Officer ……. Signature ……

Designation …….

Station & Official Stamp……... Date …….

Sharti mtoto apimwe kikamilifu kabla ya daktari kujaza fomu hii. Ikigundulika kuwa daktari alijaza fomu hii bila vipimo kufanyika, wahusika watachukuliwa hatu za kisheria na za ukiukaji wa haki za binadamu.